Ĉie fratojn mi jam multajn trovas;
Ĉar solviĝis tutmonda demando,
Homo homon ekkompreni povas.

29.II.05.

A, Dombrovski

*Fonto : Ruslanda Esperantisto,
1905.*

KIESPERANTO - SOMO LA NANE

KIONESHI CHA MWELEKEO –N

Kwa kuonesha mtendewa, tunatamatisha neno kwa **-n**. Tunasema kwamba neno hili ni katika *akuzativo*. Tunapata kioneshi cha mtendewa kwa kuuliza swali **“nani”** au **“nini”** baada ya kitenzi.

Mfano: Mi lernas Esperanton – Ninajifunza kiesperanto.

Akuzativopia hutumika kuonyesha mabadiliko ya mahali. Tunaongeza **-n** kwa jina la mahali tunapoelekea.

Mifano:

La kato saltas sur la tablon – Paka anaruka juu ya meza (akitoka chini).

Kien vi iras? – Unaenda wapi?

Venu tien ĉi – Njoo hapa.

Angalia:

Vihusishi **al** (kwa, kuelekea) na **ĝis** (hadi), ambavyo vyenyewe vinaonesha *mwelekeo*, lazima visifuatwe na *akuzativo -n*.

Mifano:

Mi iras al Daresalamon – Naenda Dar es Salaam

Iru ĝis la pordon – Nenda hadi mlangoni

Iru al la pordon – Kwenda mlangoni.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati uj-o kinamaanisha: kilicho na, ambacho hubeba.

Mono	Pesa	Monujo	Pochi
Supo	Supu	Supujo	Bakuli la supu

Kiambishi tamati hiki pia hutumika **kutaja nchi** na **miti**.

Germano	Mjerumani	Germanujo	Ujermani
Tanzano	Mtanzania	Tanzanujo	Tanzania
Mango	Embe	Mangujo	Mti wa maembe

Lakini pia tunaweza kusema:

Tanzanlando (au Tanzanio)	Jamuhuri ya mwungano wa Tanzania
Mangarbo	Mti wa maembe

Kiambishi tamati ad-i huonesha kitendo cha muda mrefu, **ad-o** ni muda wa kitendo.

Paroli	Kuongea	Paroladi	kuongea sana
---------------	---------	-----------------	--------------

Promeni	Kutembea	Promenado	kutembea, matembezi
----------------	----------	------------------	------------------------

ALIAJ VORTOJ – MANENO MENGINE

Franco	Mfaransa	Ĵeti	Kutupa
Hispano	Mhispania	Bruĭ	Kupiga kelele
Glaso	Glasi, bilauri	Naĝi	Kuogelea
Biero	Bia	Trinki	Kunywa
Plafono	Dari	Flugi	Kupaa
Muro	Ukuta	Iri	Kwenda
Tero	Ardhi, dunia	Eniri	Kuingia
Sidi tere	Kukaa chini	Eliri	Kutoka
Patrujo	Nchi (ya baba)	Levi	Kuinua
Papilio	Kipepeo	Leviĝi	Kusimama, kuinuka
Insekto	Mdudu	Donaci	Kutoa zawadi
Pinto	Ncha, mwisho	Fali	Kuanguka
Kelnero	Mhudumu	Manĝi	Kula
Mieno	Mwonekano, sura	Fiere	Kwa kiburi, fahari
Kolero	Hasira	Subite	Ghafla
Civilizita	Mstaarabu	Ĉirkaŭ	Karibu
Tuta	Nzima	Ĉirkaŭi	Kuzunguka
Kontenta	Kuridhika	Tra	Kupitia
Trankvila	-enye kutulia	Parkere	Kwa moyo
Ĝoja	-enye furaha	Kompatinda	Mwenye Kusikitisha
Libera	Huru		
Liberigi	Kuweka huru		
Reciti	Kukariri		

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. La infano ploras ĉar ŝi perdis la pupon kiun ŝia onklino donacis al ŝi.
 2. Ne restu ĉe la pordo, eniru aŭ eliru. 3. Diru al mi la nomojn de la objektoj kiujn mi vidas ĉirkaŭ vi. 4. Granda kaj belega ĝardeno ĉirkaŭas nian domon. 5 Ne faligu la glasojn.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Je, ungependa kunywa nini? 2. Sikupata muda wa kujifunza kwa sababu nilikuwa mgonjwa sana, lakini nitajifunza kesho. 3. Unazungumza Kieperanto vizuri kama jirani yako. 4. Glasi hii ni chafu, usiweke mezani. 5. Usitupe mkate sakafuni. 6. Ubao umetengenezwa kwa mbao.

KIESPERANTO - SOMO LA TISA

VITENZI (MWENDELEZO) – SUBJUNKTIVO

Katika Kiesperanto, subjunktivo huishia kwa **u**, kama ile ya sharti.

Ke mi estu	Kwamba niwe	Ke ĝi estu	Kwamba iwe
Ke vi estu	Kwamba uwe	Ke ni estu	Kwamba tuwe
Ke li estu	Kwamba awe	Ke vi estu	Kwamba muwe
Ke ŝi estu	Kwamba awe	Ke ili estu	Kwamba wawe

Baada ya vitenzi **voli, peti, deziri, bezoni, esti necese**, kiambishi-amri **u** hutumika wakati vitenzi hivi vinafuatwa na kiunganishi **ke**.

Mifano:

Li deziras ke mi parolu u kun li	<i>Anataka niongee naye</i>
Mi volas ke vi kantu	<i>Nataka uimbe</i>
Estas necese ke vi faru vian taskon	<i>Lazima ufanye kazi yako.</i>

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati aĵ-o kinamaanisha kitu.

Nutri	Kulisha	Nutra ĵo	Chakula
Trinki	Kunywa	Trinka ĵo	Kinywaji
Manĝi	Kula	Manĝa ĵo	Chakula

NUTRAĴOJ 1 – VYAKULA 1

Faruno	Unga	Frukta	-a matunda
Kuko	Keki	Fruktodona	-enye matunda
Biskvito	Biskuti	Butero	Siagi
Legomo	Mboga	Salo	Chumvi
Terpomoj	Viazi	Sukero	Sukari
Fazeoloj	Maharage	Sukeri	Kutia sukari
Salato	Saladi	Akvo	Maji
Rizo	Mchele	Teo	Chai
Fruktoj	Matunda	Kafo	Kahawa

MANENO MENGINE

Kulero	Kijiko	Mola	Laini
Forko	Uma	Malmola	Ngumu
Telero	Sahani	Muro	Ukuta

Preta	Tayari	Deziri	Kutamani, kutakia
Bongusta	Tamu	Vivi	Kuishi
Ŝati	Kupenda	Permesi	Kuruhusu
Mateno	Asubuhi	Proponi	Kutoa
Tagmanĝo	Chakula cha mchana	Devi	Kulazimika
Vespermangô	Chakula cha jioni	Estas necese	Ni lazima
Sati	Kushiba	Io	Kitu fulani
Soifi	Kuwa na kiu	Sufiĉe da	Ya kutosha
Tranĉi	Kukata	Tro da	Nyingi mno
Tranĉilo	Kisu	Baldaŭ	Hivi karibuni
Tranĉaĵo	Kipande	Antaŭ ol	Kabla
Alporti	Kuleta	Restoracio	Mgahawa
		Nutri	Kulisha

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Ĉu vi volas ke mi alportu al vi kafon aŭ lakton? 2. Mi preferas lakton.
3. La hundo ŝajnas soifi, alportu al ĝi akvon por ke ĝi povu trinki. 4. Ĉu ni baldaŭ manĝos? Mi tre malsatas. 5. Estas necese ke vi purigu viajn manojn antaŭ ol manĝi. 6. Tiu frukto ne estas sufiĉe matura, prenu alian. 7. Oni devas manĝi por vivi, ne vivi por manĝi. 8. Diru al mi tion kion vi matenmanĝis.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. MKate uliokatwa. 2. Tafadhali nisaïdie kuosha sahani na kuzikausha.
3. Kama kinywaji, nataka unipe maziwa au maji. 4. Rafiki yangu na mimi tungependa kula chakula cha jioni, unaweza kutupa chakula? 5. Bustani yetu ina miti mingi ya matunda.

HO, MIA KOR'

Ho, mia kor', ne batu maltrankvile,
El mia brusto nun ne saltu for!
Jam teni min ne povas mi facile,
Ho, mia kor'!
Ho, mia kor'! Post longa laborado
Ĉu mi ne venkos en decida hor'?
Sufiĉe! trankviliĝu de l' batado,
Ho, mia kor'!

L. L. Zamenhof

KIESPERANTO – SOMO LA KUMI

VITENZI (MWENDELEZO) – SHARTI

Masharti yanaonyesha hali na inaishia na **us** kwa Kiesperanto. sawasawa na **-nge-** kwa Kiswahili.

Mi **estus** Ninge**kuwa**
Viest**us** Unge**kuwa**
Li **estus** Ange**kuwa**
Ŝi **estus** Ange**kuwa**

Ĝi **estus** Ange**kuwa**
Ni **estus** Tunge**kuwa**
Viest**us** Mnge**kuwa**
Ili **estus** Wange**kuwa**

MATUMIZI YA “SE”

Neno **SE**linaweza kutafsiriwa kwa njia tatu tofauti:

1° kueleza hali fulani, inatafsiriwa na **se** kwa Kiesperanto, sawasawa na **kama** ya Kiswahili.

✚ **Se** vi ven**us** ni **estus** feliĉaj – **Kama** ungekuja tungefurahi.

2° ikieleza kuhojiwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja, inatafsiriwa na **ĉu**.

✚ Diru al mi **ĉu** vi venos – Niambie **kama** utakuja.

3° ikiwa na maana ya **sana** inatafsiriwa na **tiel**.

✚ Vi marŝas **tiel** rapide ke mi ne povas sekvi vin – Unatembea haraka **sana** hivi kwamba siwezi kukufuata.

SIFA KUU

Katika Kiesperanto, **zaidi ... ya** inatafsiriwa kama **plej ... el**.

• Anita estas la **plej** bela **el** ĉiuj – Anita ndiye mrembo **kuliko** wote au Anita ni mrembo **kuliko** wote.

Tazama pia:

Unu **el** tiuj homoj – Mmoja **wa** watu hawa.

Usemi “... iwezekanavyo” unatafsiri **kiel eble plej...**

Venu morgaŭ **kiel eble plej** akurate – Njoo kesho kwa wakati **iwezekanavyo**.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati –ido ina maana ya wana wa kizazi, au wana wa (kwa watu na wanyama).

Ŝafo	Kondoo	Ŝafido	Mwana-kondoo
Reĝo	Mfalme	Reĝido	Mwana mfalme
Isralo	Israeli	Israelido	Mwisraeli

Kiambishi tamati –aro kinamaanisha mkusanyiko.

Arbo – Mti

Arbar**aro** – Msitu

Esperantisto – Mwesperanto Esperantist**aro** – Waesperanto

Kiambishi -ero kinaonesha kipande, kipengele.

Fajro – Moto

Fajr**ero** – Cheche

NUTRAĴOJ 2 – VYAKULA 2

Fiŝo	Samaki	Botelo da vino	Chupa ya
Ovo	Yai		divai
Sauĉo	Mchuzi	Viando	Nyama
Vinagro	Siki	Porko	Nguruwe
Oleo	Mafuta	Porkaĵo	Nyama ya
Vino	Mvinyo, divai		nguruwe

MANENO MENGINE

Danĝera	Hatari	Servisto	Mtumishi
Opinii	Kufikiria	Iom	Kidogo
Opinio	Maoni	Iom da vino	mvinyo kidogo
Kuniklo	Sungura	Laŭ	Kulingana na,
Buĉi	Kuchinja		kwa
Buĉisto	Mchinjaji	Ne ... plu	Sivyo tena
Antaŭsciigi	Kuarifu	Soifi	Kuwa na kiu
Bonvolu	Tafadhali	Mi dankas	Nakushukuru
Akcepti	Kukubali	Dankon	} Asante
Servi	Kutumikia	Danke	
Kruĉo	Mtungi	Kelke da	} Baadhi
Korko	Kizibo	kelkaj	
Korktirilo	Kizibao	Ĉiu	Kila mmoja,
Taso	Kikombe		Kila mtu
Multe da	} Mengi, nyingi	Ĉiuj	-ote (wote, ...)
multaj		Plena	Iliyojaa
Malmultaj	-chache	Plenigi	Kujaza

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Mi petas, donu al mi glason da akvo kun iom da kafo, dankon. 2. Kion vi trinkos? Bieron, akvon, lakton, vinon, teon, kafon? 3. Mi deziras nur akvon, estas la plej bona el ĉiuj trinkaĵoj. 4. Diru al la kelnero alporti (au ke li alportu) alian glason da vino. 5. Trinku laŭ via soifo kaj manĝu laŭ via malsato. 6. Se la vetero estus bela ni irus en la ĉirkaŭaĵon de la urbo tagmanĝi kun amikoj. 7. Ne faru al la aliaj tion kion vi ne volus ke oni faru al vi.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Usitembee haraka sana, siwezi kukufuata. 2. Usijaze glasi yangu, sina kiu. 3. Tafadhali nijulishe wakati chakula cha ĵioni kiko tayari. 4. Tafadhali niletee kipande cha mkate, siagi na glasi ya maziwa. 5. Unaweza kuniambia kama hali ya hewa itakuwa ya moto (ya jua) kesho? 6. Ukitaka tungeweza kula bustanini. 7. Tafadhali nikopeshe kisu chako. 8. Sina njaa.

Maneno ya kujifunza kwa moyo

Bonan tagon

Bonan versperon

bonan nokton

Kiel vi fartas?

Mi fartas bone, dankon. Kaj vi?

Ankaŭ mi, dankon

Mi estas tre feliĉa konatiĝi kun vi

Kaj ankaŭ mi, ĝis revido.

Siku njema (mchana mwema)

Jioni njema

Usiku mwema

Habari yako? U hali gani?

Sijambo, asante. Na wewe?

Na mimi pia, asante.

Nimefurahi sana kukufahamu

*Na mimi pia, tuonane baadaye
(kwa heri).*

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA MOJA

MAJINA YA NAMBARI - MWENDELEZO

Kama tulivyoona katika somo la tatu, kuhesabu ni rahisi sana kwa Kiesperanto:

0 **nul**, 1 **unu**, 2 **du**, 3 **tri**, 4 **kvar**, 5 **kvin**, 6 **ses**, 7 **sep**, 8 **ok**, 9 **naŭ**, 10 **dek**, 11 **dek unu**, 20 **dudek**, 25 **dudek kvin**, 30 **tridek**, ...

Tukiongeza kwenye nambari za kardinali mwisho: **o**, **a**, **e**, tunaunda *nomino*, *vivumishi* *vya ordinal* na *vielezi*.

1° Majina

Unuo – Kitengo kimoja
Dekduo – Dazeni, kumi na mbili

2° Vivumishi vya nambari (kuonesha mpangilio, cheo)

Unua – Kwanza, -a kwanza
Dua – Pili, -a pili
Kvina – -a tano

3° Vielezi

Unue – Kwanza
Due – Pili
Trie – Tatu

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati on- hutumika kuunda nambari za sehemu.

❖ Robo ya 8 ni 2 – **Kvarono** de 8 estas 2.

Kiambishi tamati obl- hutumika kuunda vizidishi.

Duobla Mara mbili
Triobla Mara tatu
Centobla Mara mia

❖ 2 mara 3 ni 6 (**2X3=6**) hutafsiriwa kuwa: **duoble tri faras ses**.

❖ Tano mara saba ni 35 (**5X7=35**) tafsiri yake ni: **Kvinoble sep faras tridek kvin**.

❖ 11 mara 5 ni 55 (**11X5=55**) hutafsiriwa kuwa: **Dek unu oble kvin faras kvindek kvin**.

TEMPO (1) – WAKATI, MUDA (1)

Horo	Saa	Pasi	Kupita
Minuto	Dakika	La tempo pasas	
Sekundo	Sekunde		Mudaunapita
Tago	Siku	Kioma	Kiasi gani
Mezo	Katikati	Kioma horo?	Saa ngapi ?
Tagmezo	Mchana	Matene	} Asubuhi
Noktomezo	Usiku wa manane	Dum la mateno	
		Nokte	} Usiku
Horloĝo	Saa, wochi	Dum la nokto	
Brakhorloĝo	Saa ya mkononi	Hodiaŭ matene	Asubuhi hii
Montrilo	Mshale wa saa	Morgaŭ vespere	Kesho jioni

MANENO MENGINE

Suno	Jua	Fru	Kuwahi
Gaja	Mchangamfu	Frue	Mapema
Rapidi	Kuharakisha	Malfrui	Kuchelewa
Rapidu	Harakisha	Akurate	Kwa wakati
Levi	Kuinua	Kune	Pamoja
Leviĝi	Kusimama	Kial	Kwa nini
Komenci	} Kuanza	Tial ke	Kwa hiyo
Komenciĝi		poste	Baadaye
Senkulpigi	} Kusamehe	Je	Kihusishi chenye
Pardoni			maana isiyojulikana

KIHUSISHI – JE

Kihusishi hiki hakina maana sahihi, kinatumika wakati hakuna kihusishi kingine kinachoweza kutumika.

Mifano: Je la kvara horo – Saa nne.
 Alta **je** du metroj – Mita mbili (kwenda) juu.
 Plena **je** akvo – Iliyojaa maji.

SAA

Ili kuonesha saa, tunatumia vivumishi vya nambari **unua, dua, tria, n.k.** Ikiwa kuna sehemu ya saa (dakika, robo, nusu), inaelezwa kwanza.

Mifano:

Ni saa 3:5 asubuhi, hutafsiriwa kama: *Estas kvin minutoj post la tria (horo).*

Ni 11 kamili. – *Estas la dekunua horo au estas la dek-unua.*

Ni dakika 10 kabla ya saa 3 – *Estas dek minutoj antaŭ la tria.*

Ni saa 3 na robo – *Estas kvarono post la tria.*

Ni saa ngapi? – *Kioma horo estas?*

Atakuja saa ngapi? *Je kioma horo li venos?*

Saa tatu – *Je la tria (horo).*

Njia nyingine ya kuashiria wakati:

Ni saa 3:10 asubuhi – *Estas tri horoj kaj dek minutoj.*

Ni 1:15 – *Estas la unua kaj dek kvin minutoj.*

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Hodiaŭ vespere ni vespermanĝos frue, je duono post la kvina. 2. Via brakhorloĝo ne bone funkcias; ĝi malfruas. 3. Mi multe malfruas, senkulpigu min, pardonu min. 4. Kioma horo estas nun? Estas la deka. 5. Estas duono post la sepa. 6. Estas kvarono antaŭ la deka. 7. La partoj de la tago estas: la mateno, la tagmezo kaj la vespero. 8. Kial vi kutimas veni tiel malfrue? 9. Ĉu vi scias je kioma horo leviĝas la suno? Ĉirlaŭ la sesa! 10. Kiom faras duoble kvin? Duoble kvin faras dek. 11. Kiom estas la triono de naŭdek? 12. La milito estas la plej granda el ĉiuj malfeliĉaĵoj.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Jua huchomoza asubuhi. 2. Unaweza kuja kesho? Hapana, sitapata muda asubuhi, naweza kuja tu jioni saa kumi na moja au saa kumi na moja na robo. 3. Je, ungependa uletewe chakula chako cha mchana saa ngapi? Saa 8 mchana kama kawaida. 4. Muda hukimbia unapofanya kazi. 5. Asubuhi hii ndege wanaonekana kuimba kwa furaha kuliko kawaida. 6. Kwa nini mbwa hataki kula? Kwa sababu ni mgonjwa. 7. Hatukuweza kufika mapema, tafadhali utuwie radhi. 8. Mbili mara kumi ni ngapi? 9. Mbili mara kumi ni ishirini. 10. Katika nchi za ulaya, usiku ni baridi zaidi kuliko mchana.

Bona gloro pli valoras ol oro!

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA MBILI

MATUMIZI YA VIVUMISHI VYA NAMBARI

Vivumishi **unua, dua, tria, n.k.** hutumiwa kutaja miaka, karne, ukurasa, sura, mpangilio wa wafalme, nk.

Dum la sesa de oktobro – (wakati) Oktoba 06,

yaani tarehe 06 mwezi oktoba.

Jaro mil-okcent-okdek-sepa – Mwaka wa 1887

Ni vivas en la dudek-unua (XXI^a) jarcento – Tunaishi katika
karne ya 21

Kvara paĝo – Ukurasa wa 4

Deka ĉapitro – Sura ya 10

Johano dua – Yohana wa pili

AKUZATIVO - N

Tumeona kuwa **akuzativo** hutumiwa:

1. kuashiria mtendewa (*mi lernas Esperanton*).
2. kuonesha mwelekeo (*la kato saltas sur la tablon*).

Akuzativo pia hutumika kuchukua nafasi ya vihusishi : **al, je, dum** (iliyoonyeshwa au kudokezwa).

Tutasema:

- La arbo estas alta **je** ses metroj au: La arbo estas alta ses metroj**n**. – **Mti una urefu wa mita sita.**
- **Dum** la dek-kvara de aprilo au: La dek-kvaran**n** de Aprilo
Tarehe kumi na nne Aprili.
- Li iras **al** Daresalamo au: Li iras Daresalamon**n**.
Anakwenda Dar es Salaam.

Lakini tutasema:

Hodiaŭ estas la deka de junio – Leo ni Juni 10 (au: leo ni tarehe 10 Juni).

Ĝis lundo – Tutaonana jumatatu.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati –op kinaongezwa kwa majina ya nambari ili kuonesha mkusanyiko.

Du Mbili **Duope** Pamoja, kwa jozi.

Promeni du**ope**: Kutembea wawili wawili, kutembea kwa jozi.
Ni lernas ses**ope**: Tunajifunza tukiwa wasita.

TEMPO (2) – WAKATI, MUDA (2)

Jaro	Mwaka	Ĝis morgaŭ	Hadi kesho,
Jarcento	Karne	De	Tangu, kwa, ya
Monato	Mwezi		kwa kesho
Semajno	Wiki	De tri jaroj	Kwa miaka
Aĝo	Umri		mitatu
Dato	Tarehe	De longe	Kwa muda
Antaŭ du jaroj	Miaka miwili		mrefu
	iliyopita	De kvin monatoj	
Antaŭ kvin tagoj	Siku tano		Kwa miezi mitano
	zilizopita	Ĉiu	Kila, kila mmoja
Post tri horoj	Baadaya	Ĉiujara	-a kila mwaka
	masaamatatu	Ĉiutaga	-a kila siku
Ĉirkaŭ	Takribani	Ĉiudimanĉe	Kila jumapili
Ĉirkaŭ la sesa	Takribanisaa	Foje,	Maranyingine
	sita	fojon	Mara moja
Ĝis	Hata, hadi	Kelkafoje	Pengine
Ĝis nun	Mpaka sasa		

MANENO MENGINE

Miliono	Milioni	Naskiĝi	Kuzaliwa
Miliardo	Bilioni	Naskiĝo	Kuzaliwa
Sama	Ile ile	Resti	Kubaki, kukaa
Same	Vilevile	Daŭri	Kudumu
Proksima	Karibu	Daŭrigi	Kuendelea
Pasinta	Iliyopita	Viziti	Kutembelea
Lasta	-a mwisho	Intenci	Kukusudia
For	Mbali	Inviti	Kukaribisha
Foriri	Kuondoka	Akcepti	Kupokea

La tagoj de la semajno – siku za wiki

Lundo	Jumatatu	Vendredo	Ijumaa
Mardo	Jumanne	Sabato	Jumamosi
Merkredo	Jumatano	Dimanĉo	Jumapili
Ĵaŭdo	Alhamisi		

La monatoj de la jaro – miezi ya mwaka

Januaro	Januari	Julio	Julai
Februaro	Februari	Aŭgusto	Agosti
Marto	Machi	Septembro	Septemba
Aprilo	Aprili	Oktobro	Oktoba
Majo	Mei	Novembro	Novemba
Junio	Juni	Decembro	Desemba

La aĝo – Umri

Kiun aĝon vi havas? aŭ: **Kiom-jara vi estas?** – Una miaka mingapi?

Mi havas dudek jarojn aŭ: **Mi estas dudek-jara**

– Nina (umri wa) miaka ishirini.

Mi aĝas dudek kvin jarojn – Nina miaka ishirini na tano.

La dato - Tarehe

Kiu estas la hodiaŭa dato? aŭ: **Kiu estas la dato de hodiaŭ?**

– Ni ipi tarehe ya leo?

Hodiaŭ estas la deka de Septembro – Leo ni tarehe kumi septemba.

Kiam vi naskiĝis? – Ulizaliwa lini?

Mi naskiĝis la dudek-duan de julio de la jaro dumil.

- Nilizaliwa tarehe ishirini na mbili ya Julai mwaka wa elfu mbili.

Kiu estas la dato de via naskiĝo? – Tarehe yako ya kuzaliwa ni ipi?
(Tarehe ya kuzaliwa kwako ni ipi?).

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Mi petas al vi ke vi diru al mi la daton de via naskiĝo. 2. Kiun aĝon vi havas? Mi havas dudek sep jarojn. 3. Kiom da tagoj enhavas jaro? Ĝi enhavas tricent sesdek kvin tagojn. 4. De kiam vi loĝas sur la kamparo? De longe, de ok jaroj. 5. Kiom da homoj mortigis la milito? Pli ol ses milionojn!

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Unatajaje miezi katika Kiesperanto? 2. Kitu hiki kinaitwaje? 3. mwaka una miezi kumi na miwili, wiki hamsini na mbili na siku mia tatu sitini na tano au mia tatu sitini na sita. 4. Tarehe ya kuzaliwa kwako ni ipi. 5. Mwanao John ana umri gani? 6. Atakuwa na miaka nane mwezi ujao. 7. Sijakuona muda mrefu bwana mpendwa, habari yakona familia nzima ikoje. 8. Je, umejifunza Kiesperanto kwa muda gani? Miezi minne tu. 9. Kuna magazeti ya kila siku, wiki, mwezi, mwaka n.k.

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA TATU

MATUMIZI YA “KIU (NANI, NINI)” NA “KIA (KUONESHA AINA AU UBORA)”

I. Kiu hutumiwa kuuliza tu jina la mtu, mnyama au kitu tunachozungumzia.

Mifano: **Kiu** parolas? – nani anazungumza?

Kiu venis? Estas sinjoro Ludoviko – nani alikuja? Ni Bwana Luis.

II. Kia hutumiwa kuuliza juu ya aina, ubora.

Mifano: **Kia** persono li estas? – Ni mtu gani?

Li estas tre afabla – (Yeye) ni mkarimu sana.

Kia (au: **kiel**) estas la vetero? – Hali ya hewa ikoje?

Kia hutumiwa pia kama mshangao!

Mfano: **Kia** bonkora amiko! – Rafiki mzuri!

Vitenzi vya kibinafsi

Hivi ni vitenzi vinavyotumika tu katika nafsi ya tatu, umoja.

Pluvas – Kunanyesha, inanyesha

Estas necese – Ni lazima, lazima

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi eco: huonyesha ubora.

Juna	Mdogo kwa umri	Juneco	Ujana, utoto
Amiko	Rafiki	Amikeco	Urafiki
Frato	Ndugu	Frateco	Undugu
Gentila	-enye heshima	Gentileco	Adabu

SEZONOJ – MAJIRA (MISIMU)

Printempo	Majira ya masika	Neĝo	Theluji
Somero	Majiraya joto	Hajlo	Mvua ya mawe
Aŭtuno	Majira ya kuvuna, vuli	Fulmo	Radi
Vintro	Majira ya baridi	Tondro	Ngurumo
Pluvi	Kunyesha	Fulmotondro	Dhoruba ya radi
Pluvo	Mvua	Vento	Upepo
Blovi	Kupulizia, kuvuma	Seka	Kavu
		Fali	Kuanguka

MANENO MENGINE

Koto	Matope	Kaŝiĝi	Kujificha
Urbo	Mji	Kredi	Kusadiki, kuamini
Naturo	Tabia, necha	Kompari	Kulinganisha
Floro	Ua	Okazi	Kutokea
Libertempo	Muda wa mapumuziko	Alproksimiĝi	Kukaribia
Pluvombrelo	Mwamvuli	Lasi	Kuacha, kuruhusu
Agrabla	-a kupendeza	Forlasi	Kuondoka
Afabla	-zuri, mwema	Detrui	Kuharibu
Melankolia	-enye huzuni	Pro	Kwa sababu
Veki	Kuamsha	Jam	Tayari
Vekiĝi	Kuamka	Kia	Ni aina gani
Kaŝi	Kuficha		

Badala ya *la vetero estas bela*, tunaweza pia kusema: *estas bele*– *La vetero estas bela hodiaŭ aŭ estas bele hodiaŭ* – hali ya hewa ni nzuri leo.

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Oni oftege komparas la junecon kun la printempo kaj la maljunecon kun la vintro. 2. La personoj kiuj loĝas sur la kamparo fartas multe pli bone ol tiuj kiuj loĝas en la urboj; kial do ĉiuj homoj ne forlasas la urbojn? 3. Kiel (kia) estas la vetero? Ĉu pluvas, pluvetas, pluvegas? 5. Nĝis la tutan nokton; la tuta kamparo estas blanka hodiaŭ matene. 6. Ni povas foriri, la pluvo ne plu falas. 7. Mi ne plu ŝatas tiun urbeton, ĝi estas tro malpura kaj malseka; ĝiaj stratoj estas ĉiam kotaj kaj malbonodoraj. 8. Je kioma horo ni vespermanĝos? Je kvarono post la sepa, mi kredas. 9. Kia bela sunkuŝiĝo. 10. Kiam tio okazis? Tio okazis hieraŭ vespere.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Mbona tayari unaondoka, ni saa 7:30 tu. 2. Kuna tope nyingi kwenye mtaa huu mbaya, tuendelee na mwingine. 3. Kozi ya Kiesperanto hufanyika lini? Kila Ijuma. 4. Niambie jina la majira. 5. Upepo unavuma kwa huzuni kupitia miti; majani yanageuka manjano na kuanguka, ni vuli. 6. Inaonekana mvua inaanza kunyesha. 7. Ukame uliharibu mavuno yote. 8. Nitakuwa nyumbani kabla mvua haijaanza kunyesha. 9. Huyu ni mtoto yupi? Je, yeye ni mwerevu, mwenye adabu, mwenye urafiki?

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA NNE

VISHIRIKISHI

Vishirikishini aina za vivumishi vinavyoundwa kwa njia ya vitenzi, tunaweza kuyiita pia viambishi vya vitenzi.

1° Kishirikishi tendaji (amilifu): Kinaonyesha kitendo kinachotendwa na mhusika.

Kwa mfano: Mi estas **amanta** – Mimi nina upendo, ninapenda.

2° Kishirikishi tulivu: Kinaonyesha kitendo kilichopokelewa na mhusika.

Kwa mfano: Mi estas **amata** – Napendwa.

Kitendo kinachoweza kufanywa katika wakati *uliopo*, *uliopita* au *ujao*; kuna maumbo matatu ya kishirikishi amilifu na tatu ya Kishirikishi tulivu.

Kitenzi: "kusaidia"	Kishirikishi tendaji	Kishirikishi tulivu
Nyakati		
<i>Wakati uliopo</i>	Helpanta	Helpata
<i>Hapo uliopita</i>	Helpinta	Helpita
<i>Wakati ujao</i>	Helponta	Helpota

Kitenzi kisaidizi

Katika Kiesperanto kuna kitenzi kisaidizi kimoja tu, kitenzi **kuwa**. Tuone jinsi tunavyoweza kutumia viambishi hivyo vya vitenzi. Hebu, tuchukue kitenzi **Kupenda**.

❖ **Wakati uliopo:** Mi **amas** aŭ: mi estas **amanta**
– Napenda, mimi nina upendo (yaani sijamaliza kupenda).

❖ **Wakati uliopita:** Mi **amis** aŭ: mi **estis** **amanta**
– Nilipenda, nilikuwa na upendo.

❖ **Zamani kwa muda usiojulikana:** Mi **estis** **aminta**
– Nilikuwa katika mapenzi.

❖ **Wakati ujao:** Mi **amos** aŭ: mi **estos** **amanta**
– Nitapenda (nitakuwa na upendo, nitakuwa nikipenda).

❖ **Masharti:** Mi **amus** aŭ: mi **estus** **amanta**
– Ningependa, ningekuwa na upendo.

❖ **Sharti:** Amu aŭ: **estu** **amanta** – Upende, kuwa na upendo.

Tafadhali kumbuka:

Fomu za mchanganyiko zinapaswa kutumiwa mara chache iwezekanavyo. Kwa mfano, badala ya “**mi estas amanta**” sema tu: “**mi amas**”.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati ejo: huonyesha mahali.

Lerni	Kujifunza	Lernejo	Shule
Dormi	Kulala	Dormejo	Mahali pa kulala
Labori	Kufanya kazi	laborejo	Kazini
Preĝi	Kuomba	Preĝejo	Kanisa

Kiambishi tamati em- huonyesha anayependa.

Labori	Kufanya kazi	Laborema	Mwenye bidii
Atenti	Kuangalia	Atentema	Mwangelifu, makini

LERNEJO – SHULE

Alfabeto	Alfabeti	Gvidi kurson	Kuongoza kozi
Litero	Herufi	Klara	Wazi
Vorto	Neno	Klarigi	Kueleza
Vortaro	Kamusi	Instrui	Kufundisha
Frazo	Sentensi	Instruisto	Mwalimu
Ekzerco	Mazoezi	Sukcesi	Kufanikiwa
Elparoli	Kutamka	Progresi	Kuendelea
Ekzameno	Mtihani		mbele
Scivola	Anayetaka kujua	Demandi	Kuuliza
sciema		Respondi	Kujibu
Mallaborema	Mvivu	Memori pri	Kukumbuka
Mallaboremo	Uvivu	Forgesi	Kusahau
Interparoli	Kuongea	Atenti	Kuangalia
Babili	Kuzungumza	Atentu	Uwe makini, angalia
Devigi	Kulazimisha		
Esti devigata	Kulazimishwa	Silenti	Kunyamaza
Puni	Kuadhibu	Erari	Kufanya makosa
Peni	Kufanya juhudi	Eraro	Kosa
	kukemea	Veti	Kubashiri
Riproĉi	kupongeza	Ĉeesti	Kuhudhuria
Gratuli	kuongoza	Fini	Kumaliza
Gvidi		Anstataŭ	Badala ya

Finiĝi Kumalizika,
Laŭte kwisha
 Kwa sauti
 kubwa
Jen Tazama
Jen estas Hii hapa

Jen li estas Kuyu hapa
Signifi Kumaanisha
Kion tio signifas?
 Hiyo inamaanisha nini?
Esperanta kurso
 Kozi ya kiesperanto

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. De kiu estas gvidata la esperanta kurso? De kamarado karlo. 2. Mi vetas ke morgaŭ vi estos forgesinta miajn klarigojn, ĉar vi ne atentis. Kiel kutime vi babilas anstataŭ aŭskulti. 3. La esperantaj literoj nomiĝas: a, bo, co, ĉo, do, e, fo, kaj tiel plu. 4. Estas multaj eraroj en via hodiaŭa tasko; la proksiman fojon penu atenti pli bone. 5. Estu laborema kaj atentema kaj vi certe progresos. 6. Edzo kaj edzino estas kune nomataj geedzoj. 7. Mi ne plu memoras tion kion signifas tiu vorto. 8. Kiom da lernantoj ĉeestas la esperantan kurson? Kie ĝi okazas? 9. La instruisto demandas karlon, sed Karlo ne povas respondi ĉar li ne estas lerninta la lecionon; pro tio li estas riproĉata de la instruisto.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Kozi ya Kiesperanto hufanyika wapi na lini? Ni wanafunzi wangapi wanaosoma kozi hii? 2. Kuna makosa machache sana katika kazi yako, umepata maendeleo mengi tangu miezi miwili iliyopita; ngoja nikupongeze. 3. Tafadhali weka kazi yako ya nyumbani kwenye meza hii. 4. Kwa nini hunipi yako? 5. Nitakupa Ijumaa ijayo kwa sababu sikuwa na wakati wa kumaliza. 6. Kazi yako ya nyumbani iko wapi? Hii hapa, na hii hapa ni ya kaka yangu. Hatakuja jioni hii, kwa sababu amechoka, tafadhali msamehe. 7. Watoto wote wenye akili wanatamani kujua. 8. Nalazimika kuondoka, lazima niwe nyumbani saa sita. 9. Jina la kitu hiki katika Kiesperanto ni nini? Sikumbuki.

***Manko de oro ne estas mal-honoro
 Ne venas honoro sen laboro kaj akiro sen laboro***

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA TANO

VISHIRIKI

TOFAUTI KATI YA “ATA” NA “ITA”

1° Tunatumia kivumishi ata tunapozingatia kitendo katika utimilifu wake.

Mfano: La pordo estas fermata de Johano – Mlango unafungwa na Yohana.

2° Tunatumia kivumishi ita tunapozingatia kitendo kuwa kimekamiliika.

Mfano: La pordo estas fermita, ni ne povas eniri – Mlango umefungwa, hatuwezi kuingia.

Kishirikishi amilifu na Kishirikishi tulivu mara nyingi hutumika kuunda *nomino*, inatosha kubadilisha mwisho wao kuwa **o**.

Vishirikishi	Nomino
Lernanta – kujifunza (wakati uliopo)	Lernanto – mwanafunzi
Lernonta – karibu kujifunza (wakati ujao)	Lernonto – mwanafunzi (wa kesho)
Juĝata – kuhukumiwa (wakati uliopo)	Juĝato – anaye hukumiwa, hakimu
Juĝita – kuhukumiwa (wakati uliopita)	Juĝito – aliye hukumiwa, mfungwa
Juĝota – kuhukumiwa (wakati ujao)	Juĝoto – anayekaribia kuhukumiwa

Vishirikishi-vielezi

Ikiwa tutabadilisha mwisho wa vitenzi kuwa **e**, tunaunda vielezi ambavyo hutumiwa kutafsiri **gerund**, sawasawa na **ki** ya kiswahili.

Mifano:

Ili laboras **kantante** – Wanafanya kazi **wakiimba**.

Ne manĝu **legante** – Usile **ukisoma** (au: usile usomapo).

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati an-o: huonyesha mkaaji, mwanachama, mfuasi.

Vilaço	Kijiji	Polico	Polisi
Vilaçano	Mwanakijiji	Policano	Askari polisi
Kamparo	Mashambani	Kristo	Kristo
Kamparano	Mkulima	Kristano	Mkristo

LETERO – BARUA

Mandato	Mamlaka	Anonco	Tangazo
Sciigo	Habari	Korespondi	Kuandikiana
Informo	Taarifa	Kisi	Kubusu
Kun plezuro	} Kwa furaha	Brakumi	Kukumbatia
Plezure		Ricevi	Kupokea
Poŝtkarto	Kadi ya posta	Esprimi	Kujieleza
Adreso	Anwani	Premi	Kushinikiza
Titolo	Kichwa, cheo	Manpremi	Kupeana mkono

MANENO MENGINE

Sento	Hisia	Fariĝi	Kuwa,
Ekzisti	Kuwepo		kufanyika
Batali	Kupigana	Movi	Kujongeza
Efektivigi	Kutekeleza	Movado	Mwendo,
Efektiva	Halisi		harakati
Aperi	Kuonekana	Havigi	Kutoa
Aliĝi al	Kujiunga	Artikolo	Makala
Aboni	Kujiandikisha	Sidejo	Kakao makuu
Kosti	Kugharimu	Verko	Andiko, kazi
Rakonti	Kusimulia,	Verki	Kuandika
	kusema	Flanko	Upande
Denove	Tena	Miaflanke	Kwa upande
Pere de	Kwa njia ya		wangu
Ĵus	Sasa hivi	Mono	Pesa, fedha
Kvankam	Ingawa, ijapo	Vivkondiĉo	Hali ya maisha
Sen	Bila	Voĉo	Sauti
Laŭ la vidpunkto	} Kulingana na mtazamo	Popolo	Watu
		Ĵurnalo	} Gazeti
		Gazeto	

Ĵus – usemi "**sasa hivi...**"

Mi ĵus eniris – Nimeingia hivi punde, nimeingia sasa hivi.

Kies – usemi "**ambaye...**" hutangulia kitu kilichomilikiwa.

La urbo kies nomon mi forgesis – Mji ambao nimesahau jina lake.

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

Goma, la 25an de oktobro 2023

Kara amiko,

Mi ĝojas skribi al vi denove. Mi estas tie ĉi unu semajnon.

En kelkaj tagoj mi iros al Bukavu, kun sinjorino J., kies patro konatiĝis kun vi la pasintan jaron en la esperantista grupo. Mi rakontos al vi pri pri mia restado en Goma poste.

Mi esperas ke via familio kaj vi fartas bone.

Frate via...

Tafsiri kwa Kiesperanto

Arusha, 4 Juni 2023

Rafiki mpendwa,

Nalazimika kuondoka Arusha kwa siku chache kwa sababu nimepata barua kutoka Dar es salam ikinijulisha kuwa kaka yangu Henri ambaye unamfahamu ni mgonjwa sana. Kwa sababu hii sitaweza kuhudhuria somo la Kiesperanto litakalofanyika jumatano ijayo. Tafadhali samahani.

Rafiki yako, Joe M.

VISHIRIKISHI (SOMO LA KUMI NA NNE)

La manĝ**anta** homo – la homo kiu manĝas (mtu anayekula)

La manĝ**inta** homo – la homo kiu finis manĝi (mtu aliye kula au mtu aliyemaliza kula)

La manĝ**onta** homo – la homo kiu volas manĝi (mtu anayetaka kula au mtu anayekaribia kula).

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA SITA

VITENZI REJESHI

Vitenzi rejeshi ni vile ambavyo vinaunganishwa na viwakilishi viwili vya mtu mmoja. Katika Kiesperanto vitenzi hivi vinatafsiriwa kwa njia kadhaa:

1° ikiwa mhusika hufanya kitendo na kukiunga mkono, viwakilishi viwili hutumiwa kwa ujumla, moja ambayo ni kijalizo cha moja kwa moja, lakini katika nafsi ya 3, badala ya **lin**, **ŝin**, **ĝin**, **ilin**; tunatumia kiwakilishi **sin**.

Mfano:

Lavi **sin** – Ku**ji**osha

Mi lavas **min** – Naj**ji**osha

Vi lavas **vin** – Unaj**ji**osha

Li lavas **sin** – Anaj**ji**osha

Ŝi lavas **sin** – Anaj**ji**osha

Ĝi lavas **sin** – Inaj**ji**osha yenyewe

Ni lavas **nin** – tunaj**ji**osha

Vi lavas **vin** – mnaj**ji**osha

Ili lavas **sin** – wanaj**ji**osha

2° wakati kitenzi rejeshi kinamaanisha **kuwa hivyo**, ni afadhali tutumie **iĝi**.

Riĉa

Tajiri

Riĉ**iĝi**

Kupata utajiri, kutaj**iri**ka

Unaweza pia kutumia fomu hizo mbili kulingana na chaguo lako:
Trove **sin** aŭ trove**iĝi** – Kupatikana, kuj**i**pata

Usemi: Moja na nyingine kwa kiesperanto hutafsiriwa kuwa “**unu la alia**”.

- Ni helpas nin **unu la alian** – Tunasaidiana.
- Amu vin **unu la alian** aŭ: Amu vin **unu reciproke** – pendaneni, mpendane ninyi kwa ninyi.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati ebla: huonyesha uwezekano.

Legi Kusoma

Legebla

Inayosomeka

Vidi Kuona

videbla

Inayoonekana

Fari kufanya

Farebla

inayowezezana

LA DOMO KAJ LA MEBLARO – NYUMBA NA SAMANI, FANICHA

La hejmo	Nyumba, kwetu	Malsupreniri	Kwenda chini, kushuka
Hejme	Nyumbani	Halti	Kusimama
Kastelo	Ngome, jumba	Rimarki	Kutambua
Etaĝo	Ghorofa	Dividi	Kugawanya
Sur la unua etaĝo	Kwenye ghorofa ya kwanza	Lui	Kukodisha
Teretaĝo	Sakafu ya chini	transloĝigi	Kuhama
Ŝtupo	Hatua, daraja	Endomiĝi	Kuingia ndani ya nyumba
Ŝtuparo	Ngazi	Utila	Muhimu, -a faida
Kameno	Mahali pa moto	Utili	Kuwa na faida
Tegmento	Paa	Malutila	Inayo madhara
Grenejo	Ghala	Malutili	Kudhuru
Kuirejo	Jikoni	Neutila	} Isiyo na maana
Salono	Sebule	Senutila	
Multetaĝa	-enye ghorofa nyingi	Manki	Kukosa
Tualetejo	Choo	Loki	Kuweka
Spegulo	Kioo	Loko	Mahali
Sitelo	Ndoo	Teni	Kushika, kuweka
Meblaro	Samani	Tenilo	Mpini
Ŝranko	Kabati	Ekstere	Nje
Tapiŝo	Zulia	Interne	Ndani
Vidaĵo	Mwonekano	Kredeble	Pengine, huenda labda
Rompi	Kuvunja	Tuj	Mara moja
Densa	Nene	Nek... nek	Wala ... wala
Supra	-a juu	Apud	Karibu na
Supreniri	Kwenda juu	Kontraŭ	Dhidi ya

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Ne foriru tuj, ĉar kredeble pluvos post ne longe. 2. Tuj kiam mi estos endomiĝinta, mi petos vin viziti min. 3. La domo kies tegmenton vi vidas malantaŭ tiuj arboj, apartenas al mia avo kaj estas konstruita de li. 4. Kvankam li ĵus tagmanĝis, li ankoraŭ malsatas.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Kiti hiki kimevunjika, unaweza kunipa kingine? 2. Nilisahau pochi yangu chumbanikwangu kwenye ghorofa ya pili; je ungependa kunichukulia? 3. Ninataka kuhama haraka iwezekanavyo. 5. Njoo sasa, nahitaji unisaidie kubeba viti hivi nyumbani na kiti hiki kilichoharibika ndani ya bustani. 6. Ameondoka.



KANTO: BONVENON AL LA 109-A UNIVERSALA KONGRESO DE ESPERANTO



1. Alvenis finfine la tag'
atendita en Afriko jar-dekojn ;
ĉi-jare, flirtos la Esperanto-flag'
en Tanzanio por signi pacon al Afrik'
El la tuta mondo l'esperantistar'
bonvenas al la lando de alt-pinta montar', *Kilimanĝaro*;

Riĉa faŭne kaj flaŭre, Tanzanio,
Riĉa faŭne kaj flaŭre, Tanzanio.

Refreno :

La Afrika esperantistaro diras al ĉiuj:
Bonvenon al Afriko!
Bonvenon al Tanzanio, la 109-a kongresland',
al Aruŝo, la gast-ama urbo,
Se vi ankoraŭ ne aliĝis, rapidu.

2. Prelegoj, ekskursoj, konkursoj, ludoj, konatiĝoj
kun la afrika kulturo en amika etoso,
jen la ĉefaj trajtoj de la ĉi-jara kongreso,
Karaj samideanoj, el la tuta mondo
ne maltrafu la unuan, unikan UK-on,
okazon ĝui la Afrikan gast-am'econ,

Kaj ekscii multon pri nia kontinento;
Kaj ekscii multon pri nia kontinento.

***Teksto kaj muziko : Joe Mo (Joel Muhire),
Trovu ĝin en jutubo.***

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA SABA

KIVUMISHI KIMILIKISHI KIREJESHI SIA

Sia ina maana: **-ake, -ao**. Kwa kawaida tunaitumia badala ya: **lia, ŝia, ĝia, ilia**; mbele ya kitu kilichomilikiwa katika sentensi.

Kazi yake:

1° **Sia** lazima isitangulie jina.

Mfano: Ndugu **yake** alikuja: **Sia, lia** patro venis.

2° **Sia** inatumika tu kabla ya kitu kinachomilikiwa na mhusika wa sentensi ya pili.

Mfano:

Paka anacheza na mtoto **wake** – La katino ludas kun **sia** ido.

Kumbuka: kivumishi **-ake, ...** kinapowekwa mbele ya kitu kilicho na mhusika katika pendekezo lingine, haipaswi kutafsiriwa kama **sia** bali kama **lia, ŝia, ĝia, ilia**.

Mfano: Paulo anasema kwamba taa **yake** iko juu ya meza yake.

1. Paulo (*jina*) anasema kwamba,

2. Taa yake (*jina*) iko juu ya meza yake.

• *Kwa hivyo tafsiri ya sentensi hii itakuwa:*

Paulo diras ke **lia** lampo estas sur **lia** tablo.

Katika usemi wa kielezi **siatempe** (kwa wakati wake), kivumishi kimilikishi **sia** kwa namna fulani hupoteza maana yake ya asili.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi awali ek: huonyesha mwanzo wa kitendo.

Kanti	Kuimba	Ekkanti	Kuanza kuimba
Manĝi	Kula	Ekmanĝi	Kuanza kula

Kiambishi awali re: huashiria marudio ya kitendo.

Fari	Kufanya	Refari	Kufanya upya
Legi	Kusoma	Relegi	Kusoma tena
Doni	Kutoa	Redoni	Kurudisha

Kiambishi awali dis: inaonesha mtawanyiko, utengano.

Ĵeti	Kurusha, kutupa	Disĵeti	Kutawanya
Iri	Kuenda	Disiri	Kutawanyika

LA URBO – MJI

Monumento	Mnara
Konstruaĵo	Jengo
Kafejo	Mgahawa
Vendejo	Duka
Vojo	Barabara
Fervojo	Reli
Vojaĝo	Safari
Sonori	Kupigia
Sonorilo	Kengele
Sonorilejo	Mnara wa kengele

Noktiĝas	Usiku unakuja
Tagiĝas	Kumekucha
Bruli	Kuungua, kuunguza
Ekbruligi	Kuwasha
Estingi	Kuzimisha
Iu	Mtu fulani
Laŭiri straton	} Kufuata njia
Trairi straton	
Iom post iom	Hatua kwa hatua

MANENO MENGINE

Tie malproksime	Mbali huko
Tie supre	Huko juu
Tie kaj tie ĉi	Hapa na pale
Eĉ	Hata
Ĉu ne?	Sivyo?
Lerta	Mwerevu, hodari
Tedi	Kuchosha
Kreski	Kukua
Kreskaĵo	Mmea
Priskribi	Kuelezea
Gliti	Kuteleza
Uzi	Kutumia
Lumi	Kuangaza
Lumigi	Kuwasha
Lunlumo	Mwanga wa mwezi
Brili	Kumetameta
Zumi	Kupiga kelele
Boji	Kubweka
Miaŭi	Kulia miau
Bleki	Kulia (wanyama)
Bovbleki	Kulia kwang'ombe
Ŝafbleki	Kulia kwakondoo
La universo	Ulimwengu

Ĉielo	Mbingu, anga
Nubo	Wingu
Nebulo	Ukungu
Stelo	Nyota
Luno	Mwezi
Ponto	Daraja
Rivero	Mto
Riverego	Mto mkubwa
Herbo	Nyasi
Greno	Nafaka
Hirundo	Mbayuwayu
Nesto	Kiota
Monto	Mlima
Monteto	Kilima
Pejzaĝo	Mandhari
Dorno	Mwiba
Ĉarma	-a kupendeza
Kurioza	-a kutaka kujua
Plugi	Kulima
Falĉi	Kukata
Semi	Kupanda
Flui	Kutiririka
Flue	Kwa ufasaha

Matumizi mengine

1° Mem: inaonesha ubinafsi, mwenyewe.

Mifano:

Mi *mem* – mimi *mwenyewe*.

Ni *mem* venos kun ili – tutakuja nao *wenyewe*.

2° Sama: inaonesha kuwa na maana ya kufanana, ile ile.

Mifano:

La *samaj* personoj – watu walewale.

Ĉiuj homoj estas *samaj* – watu wote ni sawa.

3. Eĉ: hata.

Mifano:

Eĉ mi – hata mimi.

Li *eĉ* ne komprenas – hata haelewi.

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Petro ĵus komencis sian taskon, li eliros nur kiam lia tasko estos finita. 2. Vidu la katinon kaj ŝiajn idojn kiuj rigardas sin en la spegulo. 3. Ekpluvas, ekrepluegas. 4. Ĉu Henriko diris al vi ke lia frato estas venonta por viziti vin la proksiman sabaton? Li kredeble venos kun sia edzino. 5. Ekbruligu la lampon de la salono kaj estingu tiun de la kuirejo. 6. Kiuj estas la ĉefaj iloj kiujn oni uzas por la kamplaboroj?. 7. Oni uzas plugilojn, plugŝovelilojn kaj tiel plu. 8. La hundo bojas, la kato miaŭas, la insekto zumas, la birdoj kantas, la aliaj bestoj blekas; ŝafblekas, bovblekas, azenblekas kaj tiel plu.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Usitupe vipande vya karatasi hapa na pale kwenye zulia (tapiŝo). 2. Kanisa ambalo mnara wake unauona huko ni mnara wa kustaajabisha sana wa karne ya kumi na sita, kwa hivyo nenda ukautembelee upatapo wakati. 3. Safari njema, rafiki mpendwa. 4. Bwana M. atakuja kesho jioni na mkewe. 6. Usiku utakuja hivi karibuni, ona, nyota zinaanza kuangaza. 7. Hakuna waridi bila miiba. 8. Niambie kituo kiko upande gani. 9. Jua linaenda kutua.

HUMURAĴO

Unu viro iris en la bazaron kaj starigis antaŭ la fruktovendistino.

Li salutis kaj demandis, ĉu vi konas min?

La vendistino respondis: ne, mi ne konas vin.

Tiu viro diris al ŝi, kiel vi ne konas min? Mi ja estas via kliento!

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA NANE

VIHUSISHI

Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano kati ya maneno mengine mawili.

Mfano: La libro **de** la instruisto – Kitabu **cha** mwalimu.

Vihusishi vikuu ni:

al – kwa, kuelekea
anstataŭ – badala ya
antaŭ – mbele, kabla
apud – karibu na
ĉirkaŭ – karibu
ĉe – kwa
da – wingi, kiasi
de – ya
dum – wakati, huku
ekster – nje
el – kutoka
inter – baina, katikati
je – kwa, n.k
kontraŭ – dhidi ya

kun – na
krom – mbali na hilo
per – na, kwa njia ya
for – mbali
por – kwa
post – baada ya
preter – kupita, zaidi
pri – kuhusu
pro – kwa sababu
se – kama
sub – sub
super – juu
tra – kupitia
trans – ngamboya

Vihusishi hutumika kuunda maneno mapya kwa njia ya miisho: **a, e, i, o.**

Mifano:

Aldoni Kuongeza
Aldona -a ziada
Alveni Kufika
Anstataŭi Kubadilisha
Antaŭdiri Kutabiri
Ĉeesti Kuhudhuria
Ĉirkaŭi Kuzunguka
Ĉirkaŭaĵo Mazingira
Eniri Kuingia
Eliri Kwenda nje
Enterigi Kuzika

Enteriga - a mazishi
Internacia -akimataifa
Kune Pamoja
Postkuri Kufukuza
Preterpasi Kupita
Pripensi Kufikiria
Senigi Kunyima
Senkapigi Kukata
kichwa
Trairi Kupitia
Foresti Kukosekana

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati ind-akinamaanisha kustahili.

Bedaūri	Kujuta, kulilia	Kompati	Kuhurumia
Bedaū inda	-a kusikitisha	Kompat inda	Mwenye
Bedaū inde	Kwa bahati mbaya		kusikitisha

Kiambishi tamati estr-o kinatumika kutaja yule anayeamuru.

Urbo	Mji	Urbestro	Meya
Lernejo	Shule	Lernejestro	Mwalimu mkuu

LA SOCIO – JAMII

Civilizacio	Ustaarabu	Gajni	Kushinda
Metio	Ufundi	Abomeni	Kuchukia
Lignaĵisto	Seremala	Defendi	Kutetea
Ĉasi	Kuwinda	Kaŭzi	Kusababisha
Komerco	Biashara	Kaŭzo, kialo	Sababu
Komercaĵo	Bidhaa ya kibiashara	Konsumi	Kula, kutumia
Sindikato	Chama cha wafanyakazi	Citi	Kutaja
Armeo	Jeshi	Plenumi	Kutimiza
Soldato	Askari	Estinteco	Iliyopita,
Oficiro	Afisa	Estinto	-a kale
Apoteko	Duka la dawa	Rimedo	Rasilimali
Hotelo	Hoteli	Vojo	Njia
Surskribaĵo	Maandishi	Interbatali	Kupigana
Instruado	Kufundisha	Memmortigi sin	Kujiua
Malliberejo	Gereza	Konsili	Kushauri
Propra	Mwenyewe	Mendi	Kuagiza
Propraĵo	Mali	Provi	Kujaribu
Forta	-a nguvu, imara	Provo	Jaribu, jaribio
Forto	Nguvu	Starigi	Kuanzisha, kusimamisha
Riĉa	Tajiri	Rajti	Kuruhusiwa, kuwa na haki
Konduki	Kupelekea, kuendesha	Bazi	Kwa msingi
Manki	Kukosa	Fosi	Kuchimba
		Terfosisto	Mchimbaji

Veturi	Kutembea
	kwa gari
Veturilo	Gari
Veturigisto	Dereva
Pentri	Kupaka rangi
Razi	Kunyoa
Fabriki	Kutengeneza
Fabrikejo	Kiwanda
Aresti	Kushika (mwizi)
Ŝteli, rabi	Kuiba,
	kunyanganya
Rabisto	Mwizi
Juĝi	Kuhukumu

Kondamni	Kuhukumu,
	kulaumu
Pendi	Kutundikwa,
	kunyongwa
Pendigi	Kutundika
Striki	Kufanya
	mgomo
Ambaŭ	Zote mbili,
	wote wawili
Ĉe ĉiu paŝo	Kwa kila
	hatua
Ju pli ... des pli	Kadiri
...	ndivyo

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. En la nuna socio ĉiuj homoj laboras nur por gajni monon. 2. Ju pli la civilizacio estos efektiva, des pli la homaro abomenos la militon. 3. Mi konsilas al vi aĉeti tiun libron, ĝi estas vere leginda. 4. Mi sciigas vin ke mi ankoraŭ ne ricevis la komercaĵojn kiujn vi mendis al mi antaŭ kvar tagoj. 5. La de li konstruita domo. 6. Kio estas rimarkinda en tiu urbo? 7. Helpinda mizerulo.

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Angalia, utuendeshe haraka iwezekanavyo hadi jijini. 2. Kristo alisema: usiue; lakini Wakristo wengi hawakufuata mafundisho yake na kuuana wao kwa wao. 3. Katika kila hatua ya jiji, kuna mgahawa. 4. Maafa (katastrofo) ambayo vita imesababisha. 5. Maandishi yanayotufahamisha. 6. Tafadhali nipe baadhi ya majina ya wafanyakazi. 7. Hawa ndio watu ninaowajua katika Kiesperanto: fundi viatu, mshona nguo, mwokaji mikate, seremala, mwashi, mfua makufuli, mchoraji, mfanyakazi wa mlimo, mpishi. 8. Kuhusu.

Nur rekte, kuraĝe kaj ne flankiĝante, ni iru la vojon celitan!
L.L. Zamenhof.

KIESPERANTO - SOMO LA KUMI NA TISA

MANENO RAHISI

Katika Kiesperanto kuna maneno madogo-madogo 45 (vivumishi, viwakilishi na vielezi), vinavyoitwa maneno rahisi, yenye uhusiano fulani kati yake kutoka kwa mtazamo wa muundo na maana. Katika masomo yaliyopita tumeona baadhi ya maneno rahisi:

Kiu Kio Kie Kiam Kiom (da)

Nani? Nini? Wapi? Lini? Kiasi gani? ngapi?

Maneno haya hapo juu yanaitwa **maneno ya kuhoji** na **relativu**; kwa kuondoa herufi **k**, tunaunda mfululizo wa maneno mapya **yasiojulikana**.

Iu	Io	Ie	Iam	Iom
Mtu fulani	Kitu fulani	Mahali fulani	Siku fulani	Kidogo

Na ikiwa tunatanguliza maneno yasiyo na kikomo na herufi **t**, tunaunda mfululizo wa maonyesho.

Tiu	Tio	Tie	Tiam	Tiom
Yule	Hiyo, kile	Pale, huko	Wakati ule	Kadhaa

Angalia:

Neno **ajn** lililoongezwa kwa *maneno ya kuhoji* na *maneno kwa muda usiojulikana* hutumika kutafsiri usemi kama ifuatavyo:

Iu ajn au kiu ajn	– Yeyote
Io ajn au kio ajn	– Chochote
Ie ajn au kie ajn	– Popote
Iam ajn au kiam ajn	–Wakati wowote

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi tamati -aĉo: huonyesha udhalilishaji wa kimwili.

Kiambishi awali fi: huonyesha udhalilishaji wa maadili.

Popola**aĉo**, **fi**popolo Watu wabaya

Laborista**aĉo**, **fi**laboristo Mfanyakazi mbaya

Kiambishi tamati -ĉjo kinaonesha upendo wa kipekee kwa mwanamume.

Kiambishi tamati njo kinaonesha upendo wa kipekeekwa mwanamke. Viambishi hivi viwili huwekwa katika majina, baada ya herufi yoyote.

Patro	Baba	Paĉjo	Papa
--------------	------	--------------	------

Patrino
Avino

Mama
Bibi

Panjo, patrinjo
Avinjo

Mama
Bibi

LA HOMA SPIRITO – ROHO YA MWANADAMU

Prudento	Busara	Severa	Mkali
Saĝo	Hekima	Terura	-a kutisha
Saĝa	-enye busara	Afabla	Mwema
Pasio	Shauku	Indulga	Mnyenyekevu
Virto	Wema, uadili	Senkonscia	Aliyepoteza
Febro	Homa		fahamu
Febra	-enye homa	Fari bonon	Kufanya mema
Naturo	Tabia, asili	Trudi, devigi	Kulazimisha
Sentema	Nyeti, sensitive	Logi, allogi	} Kuvutia,
Kruela	Mkatili	Delogi	

MANENO MENGINE

Fakto	Ukweli, jambo	Sopiri je	Kutamanisana
Konvinki	Kushawishi	Enui	Kuchoka
Elekti	Kuchagua	Ŝerci	Kufanya utani
Kombini	Kuchanganya	Emocii	Kupata hisia
Zorgi pri	Kutunza,	Mediti	Kutafakari
	kujali	Rakonti	Kusimulia,
Akordigi	Kupatanisha		kusema
Nepre	Hakika, bila	Dubi	Kuwa na
	shaka		shaka
Pli poste	Baadaye	Senduble	Bila shaka
Almenaŭ	Angalau	Celi	Kulenga
Kvazaŭ	Kama,	Celo	Lengo
	kana kwamba	Trafi	Kufikia lengo,
Komuna	-a pamoja		kupata
Facila	Rahisi	Serioza	Makini
Grava	Mhimu	Arto	Sanaa
Konfidi al	Kabidhi kwa	Muziko	Muziki
Songî	Kuota	Sono	Sauti
Premsonĝo	} Jinamizi	Senigi je	Kunyima
Terursonĝo		Spaco	Nafasi, eneo
		Limo	Kikomo, mpaka
		Landlimo	Mpaka wa nchi

Partiano	Mwanachama, mfuasi	Scienco	Sayansi
Bonstato	Ustawi	Pentraĵo	Uchoraji
Leĝo	Sheria	Fabelo	Hadidhi
Nombro	Nambari	Ekzemplo	Mfano
Senco	Maana	Kontraŭe	Kinyume
Sensencaĵo	Upuuzi, yasiyo namaana	Male	Chake

MAZOEZI

Tafsiri kwa Kiswahili

1. Ne konfidu al ŝajnoj. 2. Celu bone kaj vi nepre trafos. 3. Ne parolu sensencaĵojn, amiko mia. 4. Ni promenu ien ajn. 5. Ne faru malbonon al la bestoj . 6. Ĉu la homoj povas elekti siajn gepatrojn, sian korpon kaj sian spiriton?

Tafsiri kwa Kiesperanto

1. Ongea kwa umakini angalau mara moja katika maisha yako. 2. Kueleza mawazo, tunatumia maneno. 3. Usimlaumu sana. 4. Lengo la jamii liwe furaha ya wote. 5. Tusiwalazimishe wengine kwa ushauri wetu, tuwaelekeze kwa mfano wetu. 6. Ninakudai nini? 7. Usile chochote.

Malforteco ofte kaŝiĝas sub la ŝajna mildeco kaj amikeco.

KIESPERANTO - SOMO LA ISHIRINI

MANENO RAHISI - MWENDELEZO

Ikiwa tutatanguliza maneno yasiyojulikana (au yasiyo na kikomo) na herufi **ĉ**, tunaunda safu ya kukusanya:

Iu **Io** **Ie** **Iam** **Iom**

Mtu fulani	Kitu fulani	Mahali fulani	Wakatifulani	Kidogo
Ĉiu	Ĉio	Ĉie	Ĉiam	Ĉiom
Kila mtu	Kila kitu	Kila mahali	wakati wote	-ote

Ikiwa tutaweka silabi **nen-** kabla ya maneno yasiyojulikana tunapata safu ya maneno hasi, ya kukanusha:

Neniu **Nenio** **Nenie** **Neniam** **Neniom**
Hakuna mtu Hakuna kitu Si popote Kamwe Hakuna kitu

Angalia maneno mengine katika chati ya maneno rahisi 45kwenye ukurasa wa 73.

MAONI

Maneno rahisi yanaweza kuunda maneno mengine (derivaĵoj) kwa njia ya miisho ya kisarufi:

Ĉiam	- Kila mara	Ĉiama	- Daima
Tie	- Hapo, pale	Tiea	- -a huko
Kial	- Kwa nini	Kialo	- Sababu

*Usichanganye **tuta** na **ĉiu**!*

La tuta urbo - Mji mzima

Ĉiu urbo - Kila mji

- **Ĉiu** ni **ĉiuj** katika wingi, ambayo ina maana: wote...
Ĉiuj homoj - watu wote.

VORTOLISTO – MSAMIATI

Kiambishi awali eks- humaanisha zamani.

Prezidento	Rais	Eksprezidento	Rais wa zamani
Edziĝi	Kuoa	Eksedziĝi	Kuachana

Kiambishi awali el- huonyesha utimilifu kamili.

Lerni	Kujifunza	Ellerni/ <u>tut</u>lerni	Kujifunza kikamilifu
--------------	-----------	---------------------------------	----------------------

ESPERANTO - KIESPERANTO

Kunveno	Mkutano
Kunsido	Kikao
Sekretario	Katibu
Kasisto	Mweka hazina
Konsulo	Balozi
Delegito	Mjumbe
Nacio	Taifa
Civitano	Mwananchi, raia
Rilato	Uhusiano
Lingvaĵo	Lugha
Helpa lingvo	Lugha saidizi
Disvastigi	Kusambaza

Multaj	-ingi, mengi
Multenombraj	Nyingi
Simpla	Rahisi
Fama	Maarufu
Praktika	-a vitendo
Varbi	Kushawishi
Kolekti	Kukusanya
Taŭgi por	Kufaa kwa
Publikigi	Kuchapisha
Kunigi	Kuunganisha
Krei	Kuunda
Propagandi	Kueneza
Presi	Kuchapisha

MANENO MENGINE

Esti prava	Kuwa sawa, kuwa sahihi
Foresti	Kukosekana
Prokrasti	Kucheleweshwa
Senprokraste	Bila kucheleva
Ĉesi	Kukoma
Senĉese	Bila kukoma
Kotroli	Kuangalia
Klopodi	Kujaribu
Pagi	Kulipa
Senpage	Kwa bure
Ŝuldi	Kudai
Spezi	Kutumia
Elspezi	Kutumia
Enspezi	Kupata
Venki	Kushinda
Triumfi	Kushinda
Agi	Kutenda
Liveri	Kutoa
Postuli	Kudai

Birdo	Ndege
Turni	Kugeuka
Turni sin al	Kugeuka kwa
Sistemo	Mfumo
Karto	Kadi
Favoro	Fadhili
Malhelpo	Kikwazo
Fervoro	Bidii
Progreso	Maendeleo
Artikolo	Makala
Amaso	Umati
Kontraŭulo	Mpinzani
Interkompreniĝi	Kuelewana
Afero	Kitu
Prezo	Bei
Diferenco	Tofauti
Fako	Idara
Flago	Bendera
Fundamento	Msingi
Majstro	Bwana
